



Mpendwa Mzazi/Mlezi:

Tunafuraha ya kwamba wewe na familia yako ni wanachama wa jamii yetu tofauti, ambapo zaidi ya lugha 100 sasa zinazungumzwa. Shule za Umma za Prince William County zimejitolea kumpa kila mwanafunzi *Masomo ya Kiwango cha Juu*. Kwa kuwa ushirikiano wa familia ni muhimu katika utendaji huu, tunafuraha kutoa maelezo msingi ili kusaidia kila mzazi na mlezi kuelewa na kuhusika na masomo ya mtoto wao.

Nyenzo zote za shule zinatolewa katika Kiingereza; hata hivyo, sisi ufasili hati muhimu na maelezo kwa zingine zinazoitishwa sana kaitka eneo letu.

Wazugumzaji wa lugha zaidi wanaweza kunufaika kutoka kwa maelezo yaliosasishwa mara kwa mara kwenye tovuti zote za Shule ya Umma ya Prince William -.pwcs.edu-na tovuti za shule binafsi. Zote zina Zana maarufu ya Ufasili ya Google, inayotoa ufasili katika lugha zaidi ya 50. Ufasili wa kompyuta mara kwa mara sio kamili, lakini bado inatoa viungo muhimu kwa maelezo ya shule. Ikiwa huna ufikiaji wa kompyuta nyumbani, unaweza kutumia moja katika maktaba yeyote ya umma.

Cha muhimu sana, Kitengo cha Shule hutoa ufikiaji kwa wakalimani stadi ili kusaidia wazugumzaji wa lugha yeyote kuelewa hati zilizo na maelezo muhimu kuhusu haki, wajibu, matarajio za mwanafunzi na mzazi, na masuala mengine yanayohusiana na kusoma na manufaa na huduma wanafunzi wanaweza kupokea. Wakalimani wanaweza kusaidia katika mikutano ya wazazi kuhusu masuala haya ili kuhakikisha wazo la kila mtu limetolewa na kueleweka. Huduma hizi hutolewa bila gharama yeyote kwa familia

Tumia yeyote ya mbinu hizi ili kupata usaidizi unaohitaji.

- Mtandaoni- nenda kwa translations.pwcs.edu
- Wewe binafsi-tembelea shule ya mtoto wako Hakuna uwezekano ya kwamba mzungumzaji wa lugha yako atakuwa. Hata hivyo mfanyakazi atatumia bango ili kukusaidia.

Kati hali zote, utaulizwa utoe yafuatayo:

- Jina lako na jina la mtoto wako;
- Shule ya mtoto wako, darasa, na jina la mwalimu;
- Mtu ambaye (kwa jina au kazi) unataka kuzungumza naye, na kichwa cha majadiliano; na
- Namba ya simu na wakati bora ambao unaweza kufikiwa.

Ikiwa mtoto wako analeta ujumbe nyumbani kutoka shuleni ikiomba mkututano; au ungependa kupanga majadiliano na mwalimu au msimamizi mwingine wa shule, tumia mbinu zilizo hapa juu kuuliza mkalimani kusaidia na mazungumzo haya muhimu. Kuna mtu atawasiliana nawe haraka iwezekanavyo.

Uhusika wako unaweza kuleta tofauti nzuri katika masomo ya mtoto wako, na tunahamu ya kukusaidia kwa kufanya huduma hizi kupatikana kwako. Tunatumaini barua hii inaelezea kuhusu kujitolea kwa Shule za Umma za Prince William County kwa mtoto wako na kwako. Nina imani unashiriki pendo letu la kila mwanafunzi kupokea Masomo ya Kiwango cha Juu.

Wako Mwaminifu,



Daktari. Steven Walts
Msimamizi wa Shule

*Unapotembelea pwcs.edu, tafuta dunia yenye rangi.
ili kupata kurasa zilizo na maelezo yaliyofafanuliwa katika ujumbe huu.

